

Simbachawene aagiza matumizi ya Tausi

**Na Veronica Mheta,
Arusha**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kutumia zaidi Mfumo wa Ukusanyaji Mapato (Tausi) kuhakikisha kuwa kodi zinazolip-

wa na wananchi zinaingia serikalini.

Agizo hilo limetolewa wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha nne cha serikali mtandao (e-GA) chenye kaulimbiu ya 'Kuhakikisha Uzingatiaji Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa ubadilishanaji salama wa taarifa'.

"Serikali imejenga mkongo wa Taifa na mifumo mingine muhimu lakini watu

wanakwamisha mifumo hiyo na kukaa na fedha za serikali haswa kwenye mamlaka za serikali za mitaa lazima mhakikishe mfumo wa Tausi unafanya kazi katika serikali za mitaa ili kodi za wananchi zilipwe.

"Kusema mfumo upo chini ni kuweka mazingira yasiyo rafiki ya rushwa na ufanyikaji kazi usio fasaha," alisema.

Alitoa agizo kwa taasisi

zote za serikali kuingia kwenye mfumo huo wa e-GA ili kuwezesha mifumo ya serikali kusomana zaidi na kuleta tija kwa maendeleo ya wananchi.

Pia aliipongeza idara ya mahakama kujiunga na mfumo wa Tehama ambapo unatoa haki kwa wakati na kupelekea kesi mbalimbali kuendeshwa kidijitali na kuziagiza taasisi nyingine za serikali ambazo zinale-

galega kujiunga na mfumo huo.

Naye Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba alisema mamlaka hiyo imeunganisha taasisi za umma 109 na mifumo 117 imesajiliwa ikiwemo taasisi nne za haki jinai zikiwa zimeunganishwa na mfumo huo na kurahisisha utoaji huduma kwa haraka zaidi.